

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MAKAMPUNI  
YANAYOTOA MIKOPO KWA KUTUMIA MITAJI BINAFSI**

Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kama Mmamlaka ya Utoaji wa Leseni za Biashara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, iliandaa miongozo ya usimamizi wa Biashara ya kutoa mikopo kwa kutumia mitaji binafsi. Kampuni zilizopewa leseni za biashara ya aina hii zilisaini masharti ya kufanya biashara hiyo, ambayo yanamtaka mwombaji kuwasilisha tarifa za mikopo iliyotolewa kila baada ya miezi minne na pale watakapohitajiwa kufanya hivyo na Mamlaka ya Utoaji wa Leseni hizo. Utaratibu wa kuandaa tarifa hizo unapatikana katika tovuti ya Wizara- [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

Wamiliki wa makampuni yenye leseni za kutoa mikopo kwa kutumia mitaji binafsi, mnakumbushwa **kuwasilisha tarifa** kuitia anuwani na barua pepe iliyopo hapa chini kama ilivyokubalika katika masharti ya leseni zenu. Kutowasilisha tarifa hizo kutasababisha kunyang'anywa leseni ya biashara na kufungiwa kufanya biashara hii.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji,  
NSSF Water Front, Ghorofa ya 1,  
35 Barabara ya Edward Sokoine,  
S. L. P 9503,  
**11469 DAR ES SALAAM.**  
Simu: Na.+255 -2-2129111/8  
+255 -22- 2129109  
Fax:+255-22-2125832  
Email: [ps@mit.go.tz](mailto:ps@mit.go.tz) nakala:-dtm@mit.go.tz  
Website- [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)

IMETOLEWA NA

**KATIBU MKUU  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**